

MKATABA WA KUPANGISHA CHUMBA

MKATABA huu umefanyika leo hii tarehe :...15..... Mwezi.....10..... Mwaka 2023.

KATI YA

JULIUS MARWA METETI wa S.L.P 735 kwa upande mmoja wa mkataba (ambaye katika mkataba huu ataitwa "MWENYE NYUMBA"),

NA

METLA GENERAL SUPPLY CO.LTD Kampuni iliyosajiliwa Kisheria chini ya Sheria ya Makampuni sura ya 212 (ambaye katika mkataba huu ataitwa "MPANGAJI").

KWA KUWA, Mwenye Nyumba ni mmiliki halali wa Nyumba iliyopo kwenye Kiwanja 1261 Block "B" NORTH Buswelu ndani ya wilaya ya Ilemela;

NA KWA KUWA, Mpangaji amemwendea mwenye nyumba kwa nia ya kutaka kupangisha NYUMBA kwa malipo ya Kodi iliyokubaliwa katika mkataba huu na kwa mujibu wa masharti mengineyo yatayoafikiwa kwenye mkataba huu;

HIVYO BASI, MKATABA huu unashuhudia na kuthibitisha kama ifuatavyo:

1. KWAMBA, Mwenye Nyumba amepangisha Mpangaji nyumba hiyo iliyopo katika eneo lililotajwa hapo juu kwa kiasi cha kodi ya **SHILINGI ZA KITANZANIA LAKI MOJA TU (100,000/=)** kwa mwezi sawa na **TSH 7,200,000/=** kwa miaka sita (**6**) na mpangishaji anakiri kupokea kiasi hicho cha Fedha.
2. KWAMBA, mkataba ni wa miaka **Sita (6)** huu utanza Tarehe 15 mwezi oktoba 2023 hadi tarehe 14 mwezi oktoba 2029.
3. KWAMBA, Mpangaji haruhusiwi kufanya matengenezo au marekebisho yoyote katika Nyumba tajwa aliyopanga bila idhini ya maandishi kutoka kwa mwenye nyumba kwa muda watakaokubaliana.
4. KWAMBA, Mpangaji atalipia gharama za Maji, Umeme pamoja na Ada ya taka.
5. KWAMBA, Mpangaji amjulisha mwenye nyumba kwa maandishi mwanzo wa mwezi mmoja wa mwisho wa mkataba huu endapo atapenda kuendelea na mkataba huu kipindi utakapokwisha.

6. KWAMBA, Mpangaji atarudisha Nyumba kwa Mwenye Nyumba baada ya Mkataba huu kumalizika ingawa wanaweza kuingia Mkataba mpya na kwa masharti mapya.
7. KWAMBA, endapo "Mwenye nyumba" au "Mpangaji ataenda kinyume na mkataba huu na kutokea mgogoro, pande zote mbili zinahaki ya kufuata taratibu zote za kisheria.

KWA USHUHUDA na UTHIBITISHO, mkataba huu umewekwa sahihi na Mwenye Nyumba na Mpangaji mbele ya mashahidi kama inavyoonyeshwa hapa chini:

UMETIWA SAHIHI na KUTOLEWA
 na **JULIUS MARWA MATETI**
 ambaye ninamfahamu/
 ametambulishwa kwangu na.....
 ambaye namfahamu leo hiitarehe.....15.....Mwezi
 Mwaka 2023

Julius Marwa Mateti

MWENYENYUMBA

Mbele ya:

JINA: *MARIAM M. OMA*

SAHIHI: *[Signature]*

TAREHE: *15. 10. 2023*

WADHIFA: **WAKILI**



IMETIWA LAKIRI na KUTOLEWA LEO ILEMELA
METLA GENERAL SUPPLY CO.LTD ambaye
 ninamfahamu/ametambulishwa kwangu na

.....
Julius
 ambaye namfahamu leo hiitarehe.....15.....Mwezi

 Mwaka 2023

.....
MPANGAJI

JINA: *Julius C. Marwa*

SAHIHI: *[Signature]*

TAREHE: *15/10/2023*

WADHIFA: **MKURUGENZI**

JINA: Kilens Kudaha Lazer
SAHIHI: Kudaha
TAREHE: 15/10/2023

WADHIFA: **MKURUGENZI**